JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU
SERA, BUNGE, URATIBU NA WENYE ULEMAVU

# AJENDA YA UTAFITI 2026/27 – 2030/31

Imeandaliwa na:
Ofisi ya Waziri Mkuu,
Sera, Bunge, Uratibu na wenye Ulemavu,
S. L. P. 980,
Mtaa wa Posta,
40412 Dodoma – Tanzania.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA WAZIRI MKUU

### SERA, BUNGE, URATIBU NA WENYE ULEMAVU

# AJENDA YA UTAFITI 2026/27 – 2030/31

Ofisi ya Waziri Mkuu,
Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu,
S.L.P. 980,
Mtaa wa Posta,
**40412 Dodoma – Tanzania.**

# YALIYOMO

**YALIYOMO** ..........................................................................................................

**UTANGULIZI** ..........................................................................................................1

**1.1 Usuli** ..........................................................................................................1

**1.2 Malengo ya Ajenda** ..........................................................................................................2

**AJENDA ZA UTAFITI** ..........................................................................................................3

Ajenda 1: Uwezeshaji Kiuchumi..........................................................................................................3

Ajenda 2: Kuzuia na Kupunguza Athari za Maafa..........................................................................................................4

Agenda 3: Uratibu wa Sera..........................................................................................................7

Ajenda 4: Uratibu wa Shughuli za Serikali..........................................................................................................8

Ajenda 5: Uendelezaji wa Makao Makuu ya Nchi Dodoma na Mji wa Serikali Mtumba ..........................................................................................................10

Ajenda 6: Mfumo na Mbinu za Uratibu wa Malalamiko na Huduma kwa Wananchi......11

Ajenda 7: Siasa, Demokrasia na Amani..........................................................................................................12

Ajenda 8: Ufuatiliaji na Tathmini ya Utendaji wa Serikali..........................................................................................................14

Ajenda 9: Maendeleo ya Watu Wenye Ulemavu..........................................................................................................15

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli

Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ibara ya 52(1) – (3), ina jukumu la usimamiaji, udhibiti na utekelezaji wa siku hata siku wa kazi na shughuli za Serikali. Shughuli hizo ni pamoja na uratibu wa sera, usimamizi wa shughuli za Serikali Bungeni, ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa Serikali, usimamizi wa masuala ya maafa, uratibu wa masuala ya uwezeshaji kiuchumi, uratibu wa programu za kitaifa pamoja na uratibu wa masuala mtambuka ya kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiutawala.

Kwa kuzingatia majukumu hayo mapana ya kikatiba na mazingira ya sasa yenye mabadiliko kutokana na kasi ya ukuaji wa sayansi na teknolojia, ukuaji wa miji, hitaji la kuimarisha ushiriki wa wananchi katika uchumi na mabadiliko ya sera za kimataifa na tabianchi, uandaaji wa Ajenda za Utafiti za Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na wenye Ulemavu), ni hatua muhimu katika kuimarisha uwezo wa Ofisi kufanya maamuzi sahihi, kuongeza ufanisi katika utendaji wa shughuli zake na kuboresha utekelezaji wa mipango na sera za kitaifa. Aidha, ajenda hii inalenga kuwezesha na kutambua maeneo yanayohitaji kufanyiwa utafiti wa kina ili kukuza maendeleo jumuishi na endelevu, kuongeza uwajibikaji na kuimarisha mifumo ya utendaji.

Maandalizi ya agenda hii yamefanyika kwa kushirikisha Idara na Vitengo vyote vya Ofisi ya Waziri Mkuu. Aidha, yamezingatia miongozo na mikakati mbalimbali ya kitaifa na kimataifa ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, Mpango wa Nne wa Taifa wa Maendeleo 2026/27 – 2030/31 (FYDP IV), Mpango Mkakati wa Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na wenye Ulemavu ), Ajenda ya Maendeleo ya Afrika 2063 na Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 (SDGs). Uzingatiaji wa miongozo hii unalenga kuhakikisha kuwa masuala ya utafiti yanayobainishwa

yanajibu mahitaji halisi ya Serikali, yanaendana na vipaumbele vya kitaifa na kimataifa, na yanakuwa na mchango katika kuboresha uratibu wa Serikali.

## 1.2 Malengo ya Ajenda

### *1.2.1 Lengo kuu*

Kutoa mwelekeo wa maeneo ya kipaumbele yanayohitaji kufanyiwa utafiti ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

### *1.2.2 Malengo mahsusi*

(i) Kuweka vipaumbele vya utafiti vinavyoendana na Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050, FYDP IV, sera za kitaifa na Mpango Mkakati wa Ofisi ya Waziri Mkuu;

(ii) Kuimarisha ulinganifu kati ya utafiti, utungaji wa sera, mipango na utekelezaji;

(iii) Kuwezesha Idara na Vitengo vya Ofisi ya Waziri Mkuu kutekeleza majukumu yake kwa tija kwa kutumia taarifa sahihi na ushahidi wa kitaalamu;

(iv) Kuchochea ushirikiano kati ya Serikali, taasisi za utafiti, sekta binafsi, vyuo vikuu na wadau wa maendeleo katika ufanyaji wa tafiti; na

(v) Kuweka msingi wa ufuatiliaji wa utekelezaji wa ajenda za utafiti kwa kipindi cha 2026/27‑2030/31.

# AJENDA ZA UTAFITI

Sehemu hii inaeleza kwa muhtasari maeneo ya kipaumbele ya utafiti ya Ofisi ya Waziri Mkuu yanayolenga kutatua changamoto za kiutendaji, kiuchumi na kijamii pamoja na kuibua maarifa mapya yatakayoimarisha utendaji na uwezo wa Serikali katika kufanya maamuzi kwa kutumia ushahidi wa kitafiti. Ajenda hizi zinaonesha maeneo yenye umuhimu na kipaumbele yanayohitaji kuchunguzwa kwa kina katika tafiti na bunifu zitakazofanywa na Ofisi.

## Ajenda 1: Uwezeshaji Kiuchumi

Ajenda hii inalenga kutathmini kwa kina mifumo na afua za uwezeshaji wananchi kiuchumi kwa lengo la kuimarisha ushiriki wao katika shughuli za uzalishaji na kuboresha ustawi wa kaya. Utafiti utajikita katika kuchambua upatikanaji wa mitaji na huduma za kifedha, mchango wa programu za Serikali na mifuko ya uwezeshaji, pamoja na kiwango ambacho wananchi, hususan vijana, wanawake na makundi maalum, wananufaika na fursa za kiuchumi zilizopo katika sekta mbalimbali na miradi ya kimkakati ya maendeleo.

Kupitia ajenda hii, Serikali itapata ushahidi wa kisera na kiutendaji wa kuimarisha mifumo ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ili iwe jumuishi, yenye tija na endelevu. Matokeo ya tafiti yatasaidia kuboresha afua zinazolenga kuongeza kipato cha wananchi, kupunguza umaskini na kuimarisha usalama wa kiuchumi. Hivyo, ajenda hii itachangia katika kujenga uchumi jumuishi unaowaweka wananchi kama wahusika wakuu wa maendeleo ya Taifa.

***Maeneo ya Utafiti***

**(a) Ushiriki wa Watanzania katika Shughuli za Kiuchumi**

Eneo hili linalenga kutathmini kiwango, aina na ubora wa ushiriki wa Watanzania katika shughuli za kiuchumi, hususan miradi ya kimkakati, biashara, uwekezaji wa ndani na nje. Tafiti zitachambua vikwazo vya kimuundo, kisera na kiutendaji

vinavyokwamisha ushiriki huo, pamoja na kubaini maeneo yenye uwezo wa kuzalisha ajira na kuongeza kipato. Aidha, mapendekezo ya kisera na kimkakati yataibuliwa kwa lengo la kuongeza manufaa ya kiuchumi kwa Watanzania wengi.

**(b) Mifuko na Programu za Uwezeshaji Kiuchumi**

Eneo hili linalenga kutathmini ufanisi wa kiutendaji, uendelevu wa kifedha na matokeo ya Mifuko na Programu za uwezeshaji kiuchumi katika kuongeza ajira, kipato na uwezo wa uzalishaji wa wananchi. Pia, litabainisha maeneo yanayohitaji maboresho ili kuongeza tija ya uwekezaji wa Serikali katika uwezeshaji kiuchumi.

**(c) Mifumo ya Upatikanaji wa Mitaji kwa Wajasiriamali Wadogo na wa Kati**

Eneo hili linajumuisha kufanya tafiti kuhusu upatikanaji wa mikopo, huduma za kifedha na mifumo mbadala ya mitaji inayolenga wajasiriamali wadogo na wa kati. Pia, tafiti zitatathmini vikwazo vya upatikanaji wa mikopo na mitaji ili kupendekeza njia bora za kuongeza ujumuishi wa kifedha.

***Wadau Wakuu wa Utafiti***

Wadau muhimu katika ajenda hii ni pamoja na Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sekta Binafsi, Vyama vya Ushirika, Vyama vya Wajasiriamali Wadogo na wa Kati, Taasisi za Utafiti, Taasisi za Elimu ya Juu, na Wadau wa Maendeleo.

## Ajenda 2: Kuzuia na Kupunguza Athari za Maafa

Ajenda hii inalenga kuimarisha uelewa wa kitaalamu kuhusu vihatarishi vya majanga vinavyoikabili nchi na kuandaa mbinu madhubuti za kuzuia, kupunguza, kukabili na kurejesha hali baada ya maafa kutokea. Tanzania inakabiliwa na majanga ya asili na yanayosababishwa na shughuli za kibinadamu, ikiwemo mafuriko, ukame, maporomoko ya ardhi na majengo, moto, milipuko ya magonjwa na athari za mabadiliko ya tabianchi. Mabadiliko hayo yanaathiri maisha ya wananchi, miundombinu, huduma za kijamii na rasilimali za Taifa. Hivyo, upo umuhimu wa kufanya tafiti ili kubaini maeneo hatarishi,

mwenendo wa hatari na hatua bora za kupunguza athari kabla na baada ya majanga kutokea.

Kupitia ajenda hii, Serikali itapata ushahidi wa kisayansi unaohitajika kuboresha mifumo ya tahadhari za mapema, kujenga uwezo wa taasisi na jamii katika usimamizi wa maafa, na kuimarisha mifumo ya uchambuzi wa hatari kwa kutumia teknolojia za kisasa kama vile GIS na mifumo mingine ya uchambuzi wa data. Aidha, tafiti katika eneo hili zitasaidia kutathmini uhimilivu wa miundombinu muhimu, ikiwemo miradi mikubwa ya kimkakati kama SGR, mabwawa ya kuzalisha umeme, barabara na huduma za kijamii. Matokeo ya tafiti hizi yatatoa mwongozo wa kisera na kimkakati wa kujenga Taifa lenye uwezo wa kustahimili majanga, kupunguza athari za kijamii na kiuchumi, na kuongeza usalama na ustawi wa wananchi.

***Maeneo ya Utafiti***

**(a) Kuzuia na Kupunguza Madhara ya Maafa**

Eneo hili linajumuisha kufanya tafiti kuhusu mbinu za kupunguza majanga kwa kubaini kiwango cha hatari, kuimarisha miundombinu na kuandaa hatua za kinga kabla ya majanga kutokea. Pia, mbinu za kukabiliana na kurejesha hali, pamoja na tathmini za maafa baada ya majanga kutokea.

**(b) Aina za Vihatarishi na Maeneo Hatarishi**

Eneo hili linajumuisha kufanya tafiti kuhusu aina mbalimbali za vihatarishi vya maafa na maeneo yaliyo hatarini kukumbwa na majanga, ukubwa wa hatari na athari zinazoweza kutokea. Matokeo ya tafiti hizi yatasaidia kuandaa mipango na mikakati ya kuzuia na kupunguza madhara.

**(c) Mifumo ya Tahadhari za Mapema**

Eneo hili linajumuisha kufanya tafiti kuhusu ufanisi wa mifumo ya tahadhari za mapema kwa majanga mbalimbali kama mafuriko, moto, maporomoko ya ardhi na majengo na milipuko ya magonjwa. Tafiti zitajumuisha uwezo na ufanisi wa mifumo

iliyopo kutoa taarifa kwa wakati, usahihi wa taarifa na utabiri, upatikanaji wa taarifa kwa wananchi, na namna taarifa hizo zinavyotumiwa na zinavyochangia kupunguza madhara ya maafa.

**(d) Mfumo ya Ugharamiaji wa Maafa (*Disaster Risk Financing*)**

Eneo hili linajumuisha kufanya tafiti kuhusu mifumo ya kifedha inayoweza kugharamia maafa bila kuathiri utekelezaji wa shughuli nyingine za maendeleo. Tafiti zitajumuisha kutathmini vyanzo mbadala vya rasilimali za dharura, mifumo ya bima za majanga, na ushiriki wa sekta binafsi. Aidha, tafiti zitachunguza uwezo wa mifumo hiyo kuhakikisha upatikanaji wa fedha kwa wakati, kudumisha uendelevu wa kifedha wa hatua za kukabiliana na maafa, na kupunguza athari za kifedha za maafa kwa bajeti ya Serikali na uchumi kwa ujumla.

**(e) Uwezo wa Nchi katika Kuzuia, Kujiandaa, Kukabili na Kurejesha Hali Baada ya Maafa**

Eneo hili linajumuisha kutathmini uwezo wa taasisi, rasilimali watu, vifaa na fedha katika ngazi zote za Serikali kwenye mzingo mzima wa maafa. Tafiti zitahusisha uchambuzi wa mifumo ya kitaasisi, rasilimali, miundombinu, ushiriki wa jamii, na uratibu wa wadau mbalimbali katika usimamizi wa maafa. Tafiti zitabainisha mapungufu yaliyopo na kupendekeza hatua za kuimarisha ustahimilivu wa Taifa katika kukabiliana na majanga.

**(f) Maarifa ya Asili katika Kukabiliana na Majanga**

Eneo hili linajumuisha kufanya tafiti kuhusu mchango wa maarifa ya asili katika kutabiri, kuzuia, kujiandaa, kukabili na kurejesha hali baada ya majanga. Utafiti utachunguza mbinu za jadi zinazotumiwa na jamii mbalimbali, uwezo wake katika kutambua vihatarishi na namna maarifa hayo yanavyoweza kuunganishwa na mifumo ya kisasa ya usimamizi wa maafa ili kuongeza ustahimilivu wa jamii.

### (g) Athari za Mabadiliko ya Tabianchi kwa Miradi ya Kimkakati ya Kitaifa

Eneo hili linajumuisha kufanya tafiti kuhusu athari za mabadiliko ya tabianchi kwenye miradi ya kimkakati ya kitaifa, ikiwemo Reli ya Kiwango cha Kimataifa (SGR), mabwawa ya umeme na miundombinu mingine iliyo katika maeneo hatarishi. Utafiti utatathmini hatari zinazoweza kuathiri uimara, uendeshaji na uendelevu wa miradi hiyo, pamoja na hatua zinazohitajika ili kuimarisha ustahimilivu wake dhidi ya athari za tabianchi.

***Wadau Muhimu***

Wadau muhimu katika ajenda hii ni pamoja na Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Mamlaka za Serikali, Tawala za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Asasi za Kiraia, Taasisi za Utafiti, Taasisi za Elimu ya Juu, Taasisi za Huduma za Kibinadamu na Wadau wa Maendeleo.

## Ajenda 3: Uratibu wa Sera

Ajenda hii inalenga kuimarisha uwezo wa Serikali katika kusimamia na kutekeleza sera katika ngazi zote za kiutawala. Kwa kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu ina jukumu la uratibu wa utekelezaji wa sera, ufanyaji wa tafiti katika eneo hili ni muhimu ili kuchambua muundo na mifumo iliyopo ya uratibu wa sera, kubainisha changamoto, kutathmini namna sera za kisekta zinavyowiana na namna zinavyojumuisha malengo ya kitaifa ya muda mfupi, wa kati na mrefu. Hii itawezesha kuhakikisha kuwa mipango na sera zilizopo hazikinzani, hazitekelezi malengo yanayofanana na zinatoa matokeo tarajiwa kwa wananchi.

Kupitia ajenda hii, Serikali itapata taarifa sahihi za kuboresha upangaji, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya sera ili kujenga mfumo jumuishi unaowezesha mawasiliano na uwajibikaji kati ya wizara, idara, wakala na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Pia, tafiti zitasaidia kuongeza matumizi ya takwimu katika kufanya maamuzi, kuimarisha uratibu wa sera na kuhakikisha kuwa sera zinajibu ipasavyo changamoto za kijamii, kiuchumi, kiutawala na kimazingira.

***Maeneo ya Utafiti***

**(a) Utekelezaji wa Sera za Kitaifa**

Eneo hili linajumuisha kufanya tafiti na tathmini ya ufanisi wa utekelezaji wa sera katika ngazi mbalimbali ili kubaini maeneo ya muingiliano, mapungufu au migongano ya sera, changamoto za uratibu wa sera, pamoja na kiwango ambacho sera hizo zinazingatia malengo ya kitaifa ya muda mfupi, wa kati na mrefu.

**(b) Matokeo ya Utekelezaji wa Sera**

Eneo hili linajumuisha kupima matokeo na kufanya tathmini ya athari za utekelezaji wa sera kijamii, kiuchumi na kimazingira. Pia, kutathmini uwiano kati ya malengo yaliyopangwa na matokeo halisi. Utafiti utazingatia namna sera zinavyochangia kuboresha huduma za kijamii, maendeleo ya wananchi na maendeleo ya kitaifa kwa ujumla.

***Wadau Muhimu***

Wadau muhimu katika eneo hili ni pamoja na Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala za Serikali; Tawala za Mikoa,Mamlaka za Serikali za Mitaa; Taasisi za Utafiti; Taasisi za Elimu ya Juu; Wadau wa Maendeleo; na Asasi za Kiraia.

## Ajenda 4: Uratibu wa Shughuli za Serikali

Ajenda hii inalenga kuboresha mifumo, miundo na taratibu za uratibu wa shughuli za Serikali katika ngazi zote za kiutawala kuanzia ngazi ya Taifa, Sekta na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kwa kuzingatia jukumu la msingi la Ofisi ya Waziri Mkuu la uratibu wa shughuli za Serikali, ufanyaji wa tafiti ni muhimu ili kubaini na kutatua changamoto za uratibu zilizopo ikiwemo mgawanyo na mgongano wa majukumu katika taasisi za umma, ucheleweshaji wa taarifa, mawasiliano ya kiutendaji, utoshelevu wa mfumo wa uratibu wa shughuli za Serikali na kupungua kwa ufanisi katika utendaji wa Serikali.

Kupitia tafiti, Serikali itapata taarifa sahihi za kuwezesha kubuni, kuboresha na kuimarisha mifumo ya uratibu na utendaji, na kuimarisha uwajibikaji na ushirikiano wa taasisi za umma. Vilevile, matokeo ya tafiti yatachangia katika kuboresha uratibu wa mikakati na mipango ya maendeleo ya kitaifa ikiwemo Ilani ya Chama Tawala na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

***Maeneo ya Utafiti***

**(a) Mifumo ya Uratibu wa Shughuli za Serikali**

Eneo hili linajumuisha kufanya tafiti kuhusu ufanisi wa mifumo na taratibu za uratibu wa shughuli za Serikali katika Wizara, Idara, Wakala na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kubaini mapungufu na kupendekeza njia za kuboresha.

**(b) Usimamizi wa Programu za Kitaifa**

Eneo hili linajumuisha kufanya tathmini za uratibu, utekelezaji na matokeo ya programu za kitaifa kwa kuangalia mafanikio, changamoto na maeneo yanayohitaji maboresho ya kiutendaji na kisera.

**(c) Utekelezaji wa Ilani ya Chama Tawala**

Eneo hili linajumuisha kupima na kufanya tathmini ya utekelezaji wa ahadi, mipango na vipaumbele vilivyoainishwa katika Ilani ya Chama Tawala na jinsi vinavyotekelezwa na taasisi na sekta mbalimbali. Matokeo yake yatasaidia kubaini mafanikio, changamoto na mapendekezo ya kuboresha utekelezaji kwa kuendana na matarajio ya wananchi na malengo ya maendeleo ya Taifa.

***Wadau Muhimu***

Wadau muhimu katika ajenda hii ni pamoja na Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala za Serikali; Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; Chama Tawala; Sekta Binafsi; Wadau wa Maendeleo; Taasisi za Elimu ya Juu; Taasisi za Utafiti, na Wananchi

## Ajenda 5: Uendelezaji wa Makao Makuu ya Nchi Dodoma na Mji wa Serikali Mtumba

Ajenda hii inalenga kuchunguza mbinu na mifumo bora ya uendelezaji wa Makao Makuu ya Nchi Dodoma pamoja na Mji wa Serikali Mtumba kama kitovu cha shughuli za utawala, usimamizi wa Serikali na utoaji wa huduma za umma nchini. Kwa kuzingatia kuwa uhamiaji wa Serikali Dodoma ni hatua ya kimkakati inayobeba dhamira ya Serikali ya kuongeza ufanisi wa utendaji, Ofisi inahitaji kufanya tafiti ili kuchambua namna jiji na mji huo wa kimkakati vinavyoweza kukua katika mpangilio sahihi, uendelevu, uhimilivu na ubora wa huduma kwa wananchi, wadau na watumishi wa umma.

Kupitia utekelezaji wa ajenda hii, Serikali itapata taarifa muhimu za kuiwezesha kufanya maamuzi ya kimkakati kuhusu uwekezaji, upangaji miji, na uendelezaji wa miundombinu, makazi na mawasiliano. Aidha, tafiti zitachunguza fursa za matumizi ya teknolojia bunifu *(smart city solutions)*, mbinu za uendelezaji wa maeneo maalumu ya uwekezaji na nafasi ya sekta binafsi katika kuendeleza miundombinu na huduma. Matokeo ya tafiti yatasaidia Serikali kuweka misingi imara ya uendelezaji wa muda mrefu wa makao makuu ya nchi na mji wa Serikali.

***Maeneo ya utafiti***

**(a) Uwekezaji katika mji wa Serikali**

Eneo hili linalenga kutafiti fursa, mahitaji, athari na njia za uwekezaji *(modalities)* katika Mji wa Serikali Mtumba, hususan katka miundombinu ya umma, maeneo ya biashara, huduma za jamii, utalii wa mikutano, miundombinu ya kijani na teknolojia bunifu. Matokeo ya tafiti yatasaidia kubaini uendelezaji wa kisasa wa Mji wa Serikali, mbinu bora za kuvutia uwekezaji wa ndani na nje, pamoja na nafasi ya ushirikiano kati ya Serikali na sekta binafsi (PPP) ili kuharakisha maendeleo ya Mji wa Serikali.

**(b) Uhimilivu na Uendelevu wa Miundombinu Muhimu**

Eneo hili linajumuisha kufanya utafiti kuhusu uimara, uhimilivu na uendelevu wa miundombinu muhimu ya Makao Makuu ya Nchi na Mji wa Serikali dhidi ya ongezeko la watu, mabadiliko ya tabianchi na mahitaji ya kiuchumi. Tafiti zitahusisha kuchunguza ubora na ustahimilivu wa majengo (ikiwemo matumizi ya mbinu za ukaguzi usioharibu miundombinu (*non-destructive testing - NDT*) ya majengo, barabara, mifumo ya maji na umeme, TEHAMA, usimamizi wa taka, miundombinu ya usalama na huduma za kijamii. Matokeo ya utafiti yatawezesha Serikali kubaini maeneo yanayohitaji maboresho ili kuhakikisha miundombinu inaendelea kufanya kazi kwa ufanisi, kustahimili majanga na kuhimili mahitaji ya sasa na ya baadaye.

***Wadau Muhimu***

Wadau muhimu katika ajenda hii ni pamoja na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma; Halmashauri ya Jiji la Dodoma; Wizara yenye dhamana ya ardhi; Wizara yenye dhamana ya ujenzi; Wizara yenye dhamana ya nishati; Wizara yenye dhamana ya maji; Wizara yenye dhamana ya mamlaka za tawala za mikoa na serikali za mitaa; Wizara yenye dhamana ya fedha; Wizara yenye dhamana ya mambo ya ndani ya nchi; Taasisi zinazohusika na masuala ya uwekezaji na uendelezaji wa maeneo maalumu ya kiuchumi; Sekta Binafsi, Ofisi za Mabalozi; Wadau wa Maendeleo, na taasisi za utafiti.

## Ajenda 6: Mfumo na Mbinu za Uratibu wa Malalamiko na Huduma kwa Wananchi

Ajenda hii inalenga kutathmini taratibu, mbinu na mifumo ya kupokea, kushughulikia, kufuatilia na kutoa mrejesho wa malalamiko, kero, hoja na maombi ya wananchi katika ngazi zote za Serikali, kuanzia Serikali za Mitaa hadi Serikali Kuu. Mfumo wa sasa unakabiliwa na changamoto za ucheleweshaji wa huduma, ukosefu wa uwajibikaji, mgongano wa taasisi au ngazi tofauti za Serikali katika kushughulikia suala moja, na ufanisi mdogo katika kutoa mrejesho sahihi kwa wananchi. Kupitia tafiti zitakazotekelezwa katika ajenda hii, Serikali itapata taarifa sahihi za kuwezesha kubuni na kuunda mifumo jumuishi ya haraka na yenye ufanisi katika kutatua changamoto za wananchi.

***Maeneo ya Utafiti***

**(a) Mifumo ya Kupokea na Kushughulikia Malalamiko, Kero, Hoja na Maombi ya Wananchi**

Eneo hili linajumuisha kufanya utafiti kuhusu ubora, ufanisi na uendelevu wa mifumo inayotumiwa na Serikali katika kupokea, kuchambua na kushughulikia malalamiko, kero, hoja na maombi ya wananchi. Utafiti utazingatia njia za mawasiliano, muda wa majibu, uwajibikaji, ushiriki wa wananchi na uwezo wa mifumo au taratibu zilizopo kutoa suluhu za haraka na zenye tija kwa ustawi wa umma.

**(b) Ubora na Utoaji wa Taarifa za Mrejesho kwa Wananchi**

Eneo hili linajumuisha kufanya utafiti kuhusu namna taasisi za umma zinavyowasiliana na wananchi katika kutoa mrejesho kuhusu masuala mbalimbali ikiwemo hatua zilizochukuliwa kufuatia malalamiko au maombi yao. Utafiti utahusisha tathmini ya njia za mawasiliano zinazotumika, ubora, kasi, usahihi na uwazi wa taarifa ili kuimarisha uwajibikaji na ushirikishwaji wa wananchi.

***Wadau Muhimu***

Wadau muhimu katika ajenda hii ni pamoja na Wananchi; Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala za Serikali; Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; Asasi za Kiraia; Vyama vya Siasa; na Wawekezaji.

## Ajenda 7: Siasa, Demokrasia na Amani

Ajenda hii inalenga kutathmini namna mienendo ya kisiasa, hali ya demokrasia na mifumo ya utawala bora inavyochangia kudumisha amani na umoja wa kitaifa. Aidha, inalenga kuchochea tafiti za ushiriki wa wananchi katika masuala ya uongozi, demokrasia, ustawi wa kijamii, ulinzi na usalama wa Taifa.

Mabadiliko ya kijamii, kisiasa, kiuchumi, kidijitali na kikanda yanaongeza umuhimu wa mifumo thabiti ya ushirikishwaji wa wananchi katika kulinda amani ya Taifa. Hivyo, tafiti zinahitajika ili kupata taarifa sahihi za kuimarisha utengamao wa kisiasa, usimamizi wa haki, ushiriki wa makundi mbalimbali katika shughuli za kisiasa na mbinu za kuzuia na kudhibiti migogoro ya kijamii na kisiasa. Vilevile, tafiti katika ajenda hii zitajikita katika kutathmini nafasi ya vijana, wanawake na vyombo vya habari, pamoja na mchango wa teknolojia ya habari katika masuala ya kisiasa na utawala. Matokeo ya tafiti hizi yatasaidia kuimarisha misingi ya demokrasia, kudumisha amani na utulivu wa Taifa na kuimarisha uhusiano kati ya Serikali na wananchi kwa manufaa na maendeleo ya Taifa.

***Maeneo ya utafiti***

**(a) Ushiriki wa wananchi na uimara wa demokrasia**

Eneo hili linajumuisha kufanya utafiti kuhusu kiwango na aina ya ushiriki wa wananchi katika shughuli za kisiasa na kijamii, ikiwa ni pamoja na mchakato wa uchaguzi, mijadala ya kisera, uwajibikaji wa viongozi na ushiriki wa makundi mbalimbali katika maamuzi ya umma.

**(b) Mazingira ya Kisiasa Nchini**

Eneo hili linajumuisha kufanya utafiti kuhusu mazingira ya kisiasa nchini na namna yanavyoathiri umoja wa kitaifa, ikiwemo masuala yanayoweza kusababisha migawanyiko, misuguano ya kijamii na uvunjifu wa amani. Tafiti zitalenga kubaini mwenendo wa kisiasa, mitazamo ya makundi mbalimbali ya jamii na vichocheo vinavyoweza kuathiri utulivu wa nchi, ili kutoa mapendekezo ya kuimarisha umoja, mshikamano na amani.

***Wadau Muhimu***

Wadau muhimu katika ajenda hii ni pamoja na Wananchi; Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala; Vyombo vya Ulinzi na Usalama; Taasisi za Kiraia; Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; Vyama vya Siasa; Taasisi za Elimu ya Juu; na Taasisi za Utafiti.

## Ajenda 8:Ufuatiliajina Tathminiya Utendajiwa Serikali

Ajenda hii inalenga kutathmini mifumo, mbinu na uwezo wa Serikali katika kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa Serikali katika ngazi zote, kwa lengo la kuongeza ufanisi, uwajibikaji na tija. Tafiti zitajikita katika kutathmini ubora wa mifumo iliyopo, matumizi ya data katika kufanya maamuzi, pamoja na kuchunguza changamoto za kiutendaji, rasilimali watu, teknolojia, miradi kutokamilika kwa wakati na upungufu wa taarifa sahihi za utendaji.

Matokeo ya tafiti yatawezesha kuimarisha mfumo wa kitaifa wa ufuatiliaji na tathmini, kuendeleza mbinu za usimamizi kwa kuzingatia matokeo na kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika ufuatiliaji na tathmini, hivyo, kuongeza ufanisi wa utendaji wa Serikali, kuimarisha uwajibikaji na kuhakikisha kuwa rasilimali zinazotengwa katika mipango ya maendeleo zinatoa matokeo tarajiwa.

***Maeneo ya utafiti***

**(a) Utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo**

Eneo hili linalenga kupima na kutathmini kiwango na ubora wa utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo kwa kuzingatia ufanisi (muda, matumizi ya rasilimali, matokeo na athari kwa jamii), ushirikishwaji wa wadau na ufikiaji wa malengo ya kitaifa.

**(b) Uwezo wa taasisi za umma katika kutekeleza shughuli za ufuatiliaji na tathmini**

Eneo hili linalenga kutathmini uwezo wa taasisi za umma katika kupanga na kutekeleza shughuli za ufuatiliaji na tathmini pamoja na changamoto zinazokwamisha.

**(c) Mifumo ya ufuatiliaji na tathmini**

Eneo hili linalenga kutathmini ufanisi wa mifumo ya kitaifa na kitaasisi ya ufuatiliaji na tathmini. Utafiti huu utahusisha tathmini ya ufanisi wa mifumo ya kiutendaji na kiutawala (miundo) na mifumo ya kidigitali inayotumika katika shughuli za ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa shughuli za Serikali.

**(d) Huduma kwa wateja/wananchi**

Eneo hili linalenga tathmini ya upatikanaji wa huduma zinazotolewa na Serikali kwa wananchi ikiwemo urahisi wa kupata taarifa, uwajibikaji na kuridhika kwa wateja.

**(e) Utendaji wa Serikali**

Eneo hili linalenga kupima na kutathmini utendaji na uwajibikaji wa taasisi za umma, utendaji wa watumishi na tathmini ya ununuzi wa umma.

***Wadau Muhimu***

Wadau muhimu katika ajenda hii ni pamoja na Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala za Serikali; Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; Wadau wa Maendeleo; Asasi za Kiraia; Taasisi za Utafiti; Taasisi za Elimu ya Juu; na Sekta Binafsi.

## Ajenda 9: Maendeleo ya Watu wenye Ulemavu

Ajenda hii inalenga kuimarisha ustawi, ushiriki na ujumuishaji wa watu wenye ulemavu katika maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kitaifa. Pamoja na kuwepo kwa sera, sheria na programu mbalimbali, Watu wenye ulemavu bado wanakabiliwa na changamoto za upatikanaji wa fursa za kiuchumi, elimu jumuishi, mafunzo ya ufundi stadi, ajira na ushiriki katika programu za maendeleo. Aidha, yapo mapungufu katika uratibu wa masuala ya watu wenye ulemavu kati ya Taasisi za Umma na wadau mbalimbali.

Kupitia ajenda hii, tafiti zitatoa ushahidi wa kitaalamu utakaoiwezesha Serikali kuboresha sera, kuimarisha uratibu na kubuni afua jumuishi zitakazoongeza usawa,

fursa na mchango wa watu wenye ulemavu katika maendeleo ya Taifa. Matokeo ya tafiti yatasaidia kuongeza uwajibikaji wa taasisi za umma na binafsi, kuboresha upangaji wa programu na kuhakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanashiriki kikamilifu na kunufaika na jitihada za maendeleo.

***Maeneo ya Utafiti***

**(a) Ufanisi wa programu za uwezeshaji kiuchumi kwa watu wenye ulemavu**

Eneo hili linalenga kutathmini ufanisi, uendelevu na matokeo ya programu na mifuko ya uwezeshaji kiuchumi kwa watu wenye ulemavu katika kuongeza kipato, ajira na ustawi wa kaya.

**(b) Sababu na mienendo ya ulemavu nchini**

Eneo hili linalenga kubaini sababu za kiafya, kijamii, kiuchumi na kimazingira zinazosababisha au kuchangia kiwango cha ulemavu, hususan katika mikoa yenye viwango vya juu.

**(c) Uratibu wa masuala ya watu wenye ulemavu**

Eneo hili linalenga kutathmini ubora na ufanisi wa mifumo ya uratibu wa masuala ya watu wenye ulemavu katika ngazi mbalimbali za Serikali ili kubaini mapungufu na mapendekezo ya maboresho.

**(d) Matumizi ya teknolojia za kidijitali kwa watu wenye ulemavu**

Eneo hili linalenga kutathmini mchango wa zana za kidigitali katika kuboresha maisha ya kila siku kwa watu wenye ulemavu.

***Wadau Muhimu***

Wadau muhimu katika ajenda hii ni pamoja na Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala za Serikali; Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; Mashirika ya Watu Wenye Ulemavu; Taasisi za Elimu ya Juu na Mafunzo ya Ufundi Stadi; Taasisi za Utafiti; Asasi za Kiraia; Sekta Binafsi; Wadau wa Maendeleo; na Ofisi ya Taifa ya Takwimu.

